



BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 26 Mei, 2023

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

90. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Katika kuinua maisha bora ya wananchi wetu, askari wetu wa Vikosi Maalum wana mchango mkubwa wa kujenga majengo mbali mbali nchini, lakini jambo linaloshangaza ni kuona hali za makaazi yao ni duni na hairidhishi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwajengea nyumba bora za kuishi askari hawa ili kuwapunguzia makali ya maisha.

108. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Azma ya Serikali ya kujenga masoko mengi na vituo vingi vya ujasiriamali ilikwenda sambamba na dhana ya kupatikana mikopo mingi isiyo na masharti kwa wananchi ambao walitarajiwa kuyatumia masoko hayo kufanya biashara pindi wangepata mikopo hiyo. Hata hivyo, kumekuwa na mkwamo wa kupatikana mikopo iliyokusudiwa kwa kuzingatia idadi na kiwango cha upatikanaji sambamba na malalamiko ya kuwepo

kwa upendeleo katika mikopo hiyo ya wajasiriamali na wawekezaji ilhali dhana ya ujenzi ilibaki pale pale kwa idadi na ukubwa.

- (a) Je, ni ipi tathimini ya Serikali juu ya tafauti hii ya uchache wa kupatikana mitaji na wingi wa vituo vya biashara na ujasiriamali vinavyojengwa Unguja na Pemba.
- (b) Je, Serikali ina mpango gani mpya na bora wa kukabiliana na hali hiyo na kuhakikisha kwamba ujenzi unaoendelea kufanywa, una tija licha ya kutopatikana kwa mikopo kwa wananchi kama ilivyopangwa awali.
- (c) Je, Serikali haioni haja ya kubadilisha matumizi ya baadhi ya vituo vya ujasiriamali na masoko ili kulifanya soko la bidhaa liwe linahitajiwa (demanded) na lenye tija.

Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

19. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Je, Serikali italeta lini Mswada wa Sheria ya Kuziongoza Taasisi na Mashirika mbali mbali kuchangia asilimia fulani ya faida zao kwa jamii (*Corporate Social Responsibility*).

123. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Uchumi bora katika nchi yoyote hujengwa kwa kuzifanya taasisi za fedha, mabenki na taasisi za kijamii za fedha ziweze kushiriki kwa ukamilifu (pro-active) katika uchumi wa Taifa hilo. Tofauti na ilivyo Zanzibar ambayo taasisi zake hufanya biashara za kifedha.

- (a) Je, ni kwa kiasi gani Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) inashiriki katika uchumi wa Zanzibar zaidi ya kufanya biashara ya bidhaa za kifedha.
- (b) Je, ni upi mchango wa PBZ katika uchumi wa Zanzibar zaidi ya mchango wa kufanya biashara ya bidhaa za kifedha.
- (c) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuiwezesha PBZ kushiriki katika uchumi wa Zanzibar zaidi ya kufanya biashara ya bidhaa za kifedha.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

71. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuanzisha ujenzi wa barabara za ndani zenyé jumla ya kilomita 2,750 kwa Unguja na Pemba. Mradi huu ulianza rasmi tarehe 26/03/2022 na unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 40, lakini kwa bahati mbaya hadi hivi sasa bado haujaanza kwa upande wa Pemba.

- (a) Je, kuna sababu zippi zinazouzorotesha mradi huo.
- (b) Je, Serikali inatoa kauli gani ya kujengwa na kukamilika kwa haraka kwa mradi huo.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

46. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kumekuwa na mwitikio mkubwa wa wanafunzi kusoma masomo ya sayansi na wengi wa wanafunzi hao wanaojiunga na vyuo vya afya ikiwa ni pamoja na Chuo cha Afya cha Mbweni Zanzibar, hulazimika kutafuta makaazi nje ya vyuo kutokana na uhaba mkubwa wa makaazi (Accommodation) katika Chuo hicho.

- (a) Ni upi mpango wa Wizara kuongeza majengo ya makaazi ya wanafunzi (Accommodation) katika Chuo cha Afya Mbweni, ili kuleta ufanisi wa wanafunzi hao katika masomo yao.
- (b) Ni lini wataanza mchakato wa ujenzi wa majengo ya kufundishia na majengo ya makaazi ya wanafunzi ili kukidhi haja ya Wazanzibari.

II. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka 2023/2024.

Zanzibar,
26 Mei, 2023.



(Raya Issa Msellel)
KATIBU WA BARAZA